

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Wizara ya Afya

Mpango Wa Taifa wa Kifua Kikuu Na Ukoma

**REJESTA YA TIBA KINGA YA KIFUA KIKUU
(TUBERCULOSIS PREVENTIVE TREATMENT)**

KITUO. _____ HALMASHAURI. _____ MKOA. _____

REJESTA YA TIBA KINGA YA KIFUA KIKUU: TB 10

Rejesta hii inatumika kusajili wateja wote watacaoanzishiwa tiba kinga ya Kifua Kikuu katika kituo cha kutolea huduma za afya. Taarifa zinazojazwa kwenye rejesta hii zitahuishwa na zilizoko kwenye kadi ya tiba kinga ya Kifua Kikuu (TB 18). Kulingana na aina ya mteja, taarifa zingine zitahusisha kadi ya matibabu ya mgonjwa wa Kifua Kikuu (TB 01), kadi ya matibabu ya Mteja wa UKIMWI (CTC 02) na rejesta ya uchunguzi wa Kifua Kikuu kwa watu walio karibu na mgonjwa wa Kifua Kikuu (TB 17). Rejesta hii inajazwa na mtoa huduma za tiba kinga ya Kifua Kikuu aliyeko katika kituo cha tiba. Rejesta hii inatumika kufuatilia wateja wote wanaopata huduma ya tiba kinga ya Kifua Kikuu katika kituo cha tiba. Rejesta inaendelea katika kurasa mbili zinazofuatana.

Hakikisha sehemu zote zinajazwa ipasavyo

NAMNA YA UJAZAJI

Safu ya (1) Namba(serial): Andika namba mtiririko ukianza na namba 1 na kuendelea kila mwanzo wa mwaka.

Safu ya (2) Tarehe ya kusajiliwa: Andika tarehe ambayo mteja alisajiliwa kuwa anastahili kupata tiba kinga ya Kifua Kikuu kwenye kituo cha kutolea tiba

Safu ya (3) Namba ya usajili: Andika namba ya usajili

Safu ya (4) Jina: Andika majina matatu halisi ya Mteja. (Herufi kubwa)

Safu ya (5) Jinsi: Andika ME kama ni mwanamume, andika KE kama ni mwanamke

Safu ya (6) Umri: Andika umri wa Mteja kwa miaka kamili. Iwapo Mteja ana umri chini ya mwaka mmoja andika sifuri (0)

Safu ya (7) Mahali anapoishi: Andika kata, kijiji/mtaa, kitongoji anakoishi Mteja kwa sasa

Safu ya (8) Namba ya simu: Andika namba ya simu ya Mteja na namba ya simu ya msimamizi wa matibabu

Safu ya (9) Aina ya mteja: Andika namba ya kundi atokalo mteja kama ilivyoainishwa kwenye kielelezo Na. A: (1. WAVIU 2. Mtu wa karibu na mgonjwa wa TB ya mapafu 3. Mraibu 4. Mfungwa 5. Mchimbaji wa madini 6. Wengineo)

Safu ya (10) Namba ya Usajili: Andika namba ya usajili wa mteja ambaye ni MVIU kama iliyoandikwa kwenye kadi ya matibabu ya Mteja wa UKIMWI (CTC 02) au andika namba ya mgonjwa wa kifua Kikuu anayeishi na mteja kama iliyoandikwa kwenye kadi ya matibabu ya mgonjwahuyo wa Kifua Kikuu (TB 01). Iwapo mteja hahusiki na aina hizi mbili tajwa, sehemu hii iandikwe sifuri (0)

Safu ya (11) Tarehe ya kuanza dawa: Andika tarehe ya kuanza dawa katika kisanduku cha juu na aina ya dawa katika kisanduku cha chini kama ilivyoainishwa katika sehemu hiyo

Safu ya (12 hadi 20) Utumiaji wa dawa: Andika tarehe ya mahudhurio kwenye kituo cha tiba katika kisanduku cha juu, namba ya maudhi ya dawa katika kisanduku cha pili kama ilivyoanishwa kwenye kielelezo Na. B1 kwa maudhi makubwa ya dawa: (1. Ganzi kali 2. Muwasho mkali/ngozi kubabuka 3. Homa ya manjano 4. Degedege) au kielelezo Na. B2 kwa maudhi madogo madogo: (5. Vipele na muwasho vya wastani 6. Ganzi ya wastani 7. Maumivu ya tumbo 8. Kichefuchefu/kutapika), namba ya matokeo ya uchunguzi wa Kifua Kikuu katika kisanduku cha tatu kama ilivyoainishwa kwenye kielelezo Na. C: (1. Hana dalili za Kifua Kikuu 2. Anazo dalili za Kifua Kikuu), na idadi ya vidonge katika kisanduku cha chini

Safu ya (21) Tarehe ya matokeo ya matibabu: Andika tarehe ya matokeo ya matibabu

Safu ya (22) Matokeo ya matibabu: Andika namba ya matokeo ya matibabu kama ilivyoanishwa kwenye kielelezo Na. D: (1. Amemaliza 2. Ameugua Kifua Kikuu 3. Amepata maudhi ya dawa 4. Kifo 5. Utoro wa matibabu 6. Amehama 7. Ameamua kuacha matibabu)

Safu ya (23) Maoni: Andika maoni muhimu yanayomhusu mteja

